# MTIHANI WA DARASA LA NANE MUHULA WA KWANZA 2019

# KISWAHILI

**Soma vifungu hivi vina nafasi 1 mpaka 15 kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo chini. Chagua neno bora zaidi kati ya yake ukiyopewa.**

Zilikuwa habari za kusikitisha __1__ kuwa mhasiriwa wa ajali alifariki dunia baada ya hospitali __2__ jijini kuchelewa __3__. Inakasirisha kusikia kuwa iliwachukua saa kumi na nane __4__ hospitali hiyo ikaanza kumshughulikia. Kutia chumvi kwenye kidonda, hospitali nyingine ilimkataa baada ya aila ya majeruhi __5__ kushindwa kulipa shilingi elfu mia mbili. __6__ umeenda wapi? Maisha ya biandamu hayanunuliwi popote. Ni jukumu la serikali kuwalinda wanachi __7__ watu wanaoongozwa na tamaa na __8__ wa kujitajirisha huku wakiuhadaa umma kuwa wanaweza kutegemewa katika utoaji wa hudumu ya tiba.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ziliporipotiwa | B. iliporipotiwa | C. iliposema | D. iliyosemwa |
| 2. | A. kimoja | B. mmoja | C. moja | D. mamoja |
| 3. | A. kuhudumiwa | B. kuhudumia | C. kuhudumu | D. kumhudumia |
| 4. | A. ndipo | B. ndio | C. ndiyo | D. ndizo |
| 5. | A. hayo | B. huyo | C. hilo | D. hiyo |
| 6. | A. utu | B. unyama | C. huzuni | D. uhayawani |
| 7. | A. juu ya | B. zaidi ya | C. dhidi | D. dhidi ya |
| 8. | A. ukatili | B. umero | C. ulofa | D. upuuzi |

Ukakamavu __9__ msichana Lidia ulimpa nafasi ya kutoa hotuba fupi gwarideni. Alienda kuzungumzia mada __10__ zilihusu maisha ya wanafunzi shuleni aliwakumbusha wenzake umuhimu wa __11__ majukumu yao kila siku bila kuyahairisha. Alishirikia, kaulimbiu kuwa "la leo lifanye leo" na kesho ije na __12__ zake. __13__ ajabu alipendwa na walimu wote pamoja na wanafunzi alipofika darasa la saba, mwalimu mkuu alimwahidi __14__ masomo yake ya shule ya upili. Bila shaka __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. wa | B. ya | C. la | D. za |
| 10. | A. ambayo | B. ambazo | C. ambako | D. kuyashangilia |
| 11. | A. kuyatelekeza | B. kuyaambaa | C. kuyatekeleza | D. kuyashangilia |
| 12. | A. maneno | B. mambo | C. udhaifu | D. changamoto |
| 13. | A. Ni | B. Ndio | C. na | D. si |
| 14. | A. kuithamini | B. kuyathamini | C. kuyadhamini | D. kuidhamini |

15. A. chanda chema huvikwa pete  B. jung kuu halikosi ukoko
    C. dau la mnyonge haliendi joshi  D. fata nyuki nyuki uyle asali

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.**

16. Nomino '**mvua**' iko katika ngeli gani?
 A. I-I
 B. I-ZI
 C. U-I
 D. YA-YA

17. Ni sentensi ipi iliyotumia **kwa** ya sababu
 A. Watoto walienda kwa nyanya asubuhi.
 B. Wanakandanda walisafiri kwa ndege.
 C. Wakulima walisifiwa kwa bidii zao.
 D. Nyumbani kwa bwana moyo kunapendeza.

18. Maneno yaliyopigiwa vistari ni ya aina gani?
 Mtoto **wangu** amehitimu **yule** anaendelea kujiandaa kwa mtihani.
 A. Kiwakilishi, kivumishi
 B. Kielezi, kiwakilishi
 C. Kitenzi kiwajkilishi
 D. Kivumishi, kiwakilishi

19. Kamilisha kwa kiwakilishi cha idadi
 ________ hawakuhudhuria mkutano huo.
 A. Wao
 B. Wazembe
 C. Wachache
 D. Wepi

20. Chagua kinyume cha sentensi hii
 Muli alisifiwa kwa utiifu wake shuleni.
 A. Muli alikashifiwa kwa utiifu wako shuleni.
 B. Muli alikashifiwa kwa ukaidi wake shuleni.
 C. Muli alikashifiwa kwa utundu wake shuleni
 D. Muli hakukashifiwa kwa utiifu wako shuleni.

21. Mtoto wa samaki huitwa
 A. chengo
 B. kitungule
 C. bakaya
 D. nyamawa

22. Ni sentensi gani sahihi kisarufi
 A. Ningelima ningelipata mazao tele
 B. Ungalienda ungelimkuta
 C. Wangalicheza vizuri wangalishida
 D. Mwalimu angeliniita ningeliita.

23. Mstari wa tatu katika kila ubeti wa shairi la tarbia huitwa
 A. utao
 B. mleo
 C. ukwapi
 D. mlolo

24. *Chagua kielezi katika sentensi hii*
 Ndege iliyotumbukia baharini imepatikana
 A. iliyotumbukia
 B. imepatikana
 C. ndege
 D. baharini

25. Pesa zitumikazo kuanzisha biashara huitwa

A. mtaji

B. riba

C. mashurufu

D. karadha

26. Chagua usemi wa tarifa wa sentensi 'Jana niliwapa kazi gani? Mwalimu alimwuliza kiranja

A. Kiranja aliulizwa na mwalimu walipewa kazi gani

B. Mwalimu alimwuliza kiranja kazi aliyokua amewapa siku iliyotangulia

C. Mwalimu alimwuliza kiranja kazi alizowapa jana

D. Mwalimu alimwuliza kiranja niliwapa kazi gani?

27. **Andika udogo wa**

Jiwe la mwizi liliigonga meza.

A. Kijiwe cha kimwizi kilikigonga kimeza.

B. Kijiwe cha kijizi kiligonga kimeza.

C. Kijijiwe cha kijizi kilikigonga kijimeza.

D. Kijijiwe cha kimwiei kilikigonga kimeza.

28. Kamilisha nomino ya makundi.

__________ ya madola.

A. Jumuiya

B. Shehena

C. Numbi

D. Matopa

29. Binadamu aghalabu hushambuliwa na vimelea wafuatao ispokuwa;

A. kunguni

B. chawa

C. utitiri

D. funza.

30. Tegua kitendawili

Tarishi wangu huwa mfukoni.

A. rununu

B. hanchifu

C. pochi

D. kalamu

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31-40.**

Bwana Kaza alikuwa mwenye bidii kazini mwake. Bwana huyo alikuwa akifanya kazi ya ubawabu katika shule iliyoitwa Mema. Katika chumba cha bawabu kilichokuwa langoni pa shule Kaza hakukaa tu kungoja kufungulia magari wanafunzi na walimu kuingia shuleni bali pia alikuwa kila mara akisoma vitabu vya kozi ya uhasibu aliyokuwa amejisajili. Kaza alisoma kwa bidii huku akitenda kazi yake ipasavyo. Baada ya ya miaka mitatu alihitimu vizuri masomoni. Wakurugeni wa shule walipofahamishwa hayo, walifurahi ghaya na wakampandisha cheo akawa ndiye mhasibu mkuu wa shule ile. Gange hiyo mpya ilimpa Bwana Kaza donge nono. Kutokana hayo, maisha yake na ya familia yake yakachukua mkondo mpya. Changamoto zilizoiandama familia ya Kaza zikaanza kuyeyuka katika hewa yabisi.

Bwana Kaza alikuwa amemwoa mke kufu yake. Mke yule naye alifanya kazi ya uhazili katika ofisi ya chifu. Baada ya kujiandikisha katika chuo kikuu kuendeleza taaluma yake, alipandishwa daraja akawa mmoja wa wahazili katika ofizi ya gavana wa gatuzi lao.

Bidii walizokuwa nazo Bwana na Bi Kaza ziliwapa mali tele hivyo basi walijenga nyumba kubwa wakanunua mashamba na mifugo na kuwekeza hapa na pale. Kwa njia hiyo, pesa walikuwa wakiziita zinaitika.

Dayani aliwabarini wazazi hao wakamzaa mwana waliyemwita Matendekezo. Matendekezo alilelewa kwa tunu na tasha. Licha ya hayo, wazazi hao wawili hawakutaka mtu yeyote kumnyoshea mwana wao kidole cha lawama. Waliamini kuwa Matendekezo angerithi mali yao na kuendeleza kizazi chao. Kila mara walimwelekeza kuwa mali yote katika familia ingekuwa yake. Kwa sababu hiyo Matendekezo hakufanya bidii kazini wala shuleni. Masomoni, Matendekezo alidorora na kudoda, kwa sababu ya kudekezwa, kijana huyo alianza kuvimba kichwa.

Shuleni na mitaani, Matendekezo akawa ni mtoto wa kuwabughudhi wengine. Watoto wengi walipomwona walipiga mbio ana kuepuka matusi. Haukupita muda mrefu kabla ya kijana huyo kufanya kituko shuleni ni kweli kuwa ngoma ikipigwa sana hupasuka kiwambo. Siku moja baada ya kuzozana na vijana wenzake shuleni, alimpiga mmoja kwa jiwe kichwani na kumuumiza vibaya. Jambo hilo lilimfanya Matendekezo kufukuzwa shuleni. Ni wakati huo ambapo wazazi wa Matendekezo waligundua kuwa mambo yalikuwa yamemwendea tenge mwana wao kwa sababu ya malezi duni.

31. Bwana Kaza alifanya kazi zifuatazo isipokuwa
   A. kufungulia magari kuingia shuleni.
   B. kuwasajili wanafunzi shuleni
   C kuchunguza wazazi wanaoingia langoni
   D. kulinda usalama wa shule.

32. Kazi aliyoiandikisha Bwana Kaza kusomea ilikuwa ya:-
   A. unawabu
   B. ualimu
   C. utunzaji wa hesabu ya pesa
   D. uongozi wa shule

33. "Maisha yake na ya familia yake yalichukua mkondo mpya" ni maneno yenye maana kuwa
   A. alianza maisha ya ndoa
   B. maisha yake yalianza kuwa magumu sana
   C. kazi aliyafanya ilkuwa nyigni zaidi.
   D. alianza kuwa na wepesi wa kutimiza matakwa yake

34. 'Bwana Kaza alioa mke kufu yake" Hii ni kumaanisha alikuwa na
   A. mwanamke mrembo sana
   B. mwanamke aliyefuja mali sana
   C. Mwanamke mwenwye jitihada kama mume wake
   D. Mke alsiyekuwa na msimamo thabiti

35. Mshahara waliopata bwana na Bi Kaza uliwasaidia kufanya mengi makuu. Methali mwafaka kwa kauli hii ni
   A . pesa huvunja milima na nguu hulala
   B. haba na haba hujaza kibaba
   C. Asiyesikia la wakuu huona makuu
   D. Usiuone wembamba wa reli, garimosho hupita.

36. Maneno "tuni na tamasha" yaliyopigwa mfano katika ufahamu ni fani gani ya lugha?
   A. Takriri
   B. Msemo
   C. Tashbihi
   D. Istiara

37. Kiini hasa cha Matendekezo kutokuwa na bidii maishani kilikuwa ni
   A. kuzaliwa akiwa mzembe
   B. kuiga nyayo za wazazi wake
   C. kujua kauwa angekuwa mrithi wa raslimali ya wavyele wake
   D. hakupenda kuchoka.

38. Kisawe cha neno dorora ni
   A. zagaa
   B zurura
   C. zembe
   D. didimia

39. Ni jambo gani ambalo linalinganisha na ngoma iliyopigwa ikapasuka kiwambo?
   A. kutokuwa na bidii masomoni
   B. kuwa na mali tele kwa Bwana Kaza
   C. Matendekezo kuepukwa na vijana wenzake ma...
   D. Matendekezo kumdhulumu kijana mmoja na kumjeruhi

40. Funzo gani tunalopata kutokana na ufahamu huu
   A. Si vyema kuwadekeza wana katika malezi.
   B. Utajiri wa mtu hutokana na bidii zake.
   C. Watoto hawafai kurithi mali ya wazazi.
   D. Si vizuri kwa wazazi kuwapenda wana wao.

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41- 50.**

Serikali ni muhimu sana katika kila jamii. Serikali ndiyo hutoa mwongozo wa jinsi mambo yatakavyofanywa kaktika jamii hiyo. Bila serikali, jamii itajikokota sana katika kupata maendeleo. licha ya hayo. Jamii kama hiyo itajawa na mivutano na utangamano utavurugwa.

**Jamhuri** ya Kenya inayo seriklai kuu inayoongozwa na rais ambaye huchaguliwa na waopiga kura na na kuapishwa na kiongozi mkuu wa mahakama. Serikali kuu ya kenya imegawanyika katika mahakama bunge na viongozi wa idara mbalimbali za serikali.

Bunge la taifa huundwa na wabunge wanaochaguliwa na wapigakura. Jukumu kuu la bunge la taifa ni kutunga sheria zinazotumika katika kuongoza nchi. Vilevile, bunge hujadili masuala mbalimbali yanayoathiri taifa letu na kutoa maamuzi muhimu. Bunge pia husomewa makadirio ya matumzi ya fedha za serikali ili liafiki. Hivyo basi, bunge hutoa maoni na mapendekezo ya matumizi ya pesa za serikali. Mradi mbalimbali hupitishwa bungeni ili kuleta mashinani. Kiongozi wa bunge ni spika naye huchagulia na wabunge.

Katika serikali kunayo mahakama. Mahakama ndiyo ambayo hulinda sheria na haki za wananchi. Mahakama ambayo huteuliwa na rais na kuidhinishwa na bunge. Mahakama ndiyo ambayo ina idhini kisheria ya kumwadhibu yeyote ambaye anavunja sheria za nchi. Mahakama inafaa kudumisha haki na usawa kwa wote. Kunazo mahakama za aina mbalimbali, kuna mahakama za kadhi, mahakama za watoto za wanajeshi na nyinginezo. Mahamu katika mahakama hizo ndio huamua kesi tofauti.

Kila idara ya serikali inaongozwa na katibu. Katibu huyo ndiye mkuu wa idara hiyo. Idara za serikali ni kama vile. idara ya elimu, ya afya, ya kilimo na masuala ya kigeni na nyinginezo.

Makatibu wa idara hizo, wafanyakazi wote wa idara za serikali, rais na naibu wake ndio sehemu ya tatu ya serikali ya Kenya. Kazi yao ni kuhakikisha kuwa sheria zilizotungwa na bunge zimefuatw na kutekelezwa . Hapa kiongozi ni rais. Makatibu wa idara za serikali huteuliwa na rais. Polisi wote na wanajeshi hupatikana katika sehemu hii ya serikali. Sehemu hii ndiyo kuu katika serikali.

Kupitia uongozi wa serikali, jamii ya Kenya imepiga hatua kuu kimaendeleo. Nchi hii ni mojawapo ya nchi zenye uchumi, unaokua kwa kasi sana barani Afrika. Heko kwa serikali ya Jamhuri ya Kenya.

41. Chagua kauli sahihi. Bila serikali;

A. jamii haitapata maendeleo yoyote

B. shughuli za kimaendeleo zitakuwa za mwendo wa pekee

C. Jamii itakuwa kwa kasi kiuchumi

D. Jamii itajawa na utengamani na mwelekeo bora

42. Ni nani anayemwapisha rais baada ya uchaguzi mkuu?

A. mweenyekiti wa tume ya uchaguzi

B. naibu wa rais

C. spika wa bunge

D. kiongozi mkuu wa mahakama

43. Neno **Jamhuri** limepigiwa mstari katika ufahamu maaaya yake ni

A. nchi huru inayotawaliwa na rais aliyechaguliwa kidemokrasi na wanachi

B. nchi inayoongozwa na mfalme

C. nchi inayotawaliwa na rais aliye mahamakani kimabavu

D. nchi iliyotawaliwa na wakoloni.

44. Wabunge huingia vipi mamlakani?

A. Kwa kuchaguliwa na wapiga kaura

B. Kwa kuchaguliwa na wenzao

C. Kwa kuteuliwa na rais

D. Kwa kuteuliwa na tume ya uchaguzi

45. Kazi kuu ya bunge ni ipi?

A. kuafiki uteuzi wa viongozi wa idara za serikali wanaoteuliwa na rais

B. kuidhimisha matumizi ya fedha za kiserikali

C. kujadili masuala yanayoathiri nchi

D. kuunda na kutunga sheria za nchi

46. Chagua kauli sahihi kuhusu spika wa bunge

A. huteuliwa na raia kuongoza vikao vya bunge

B. kuchaguliwa na wananchi kuongoza bunge

C. huteuliwa na kiongozi mkuu wa mahakama

D. huchaguliwa na wabunge

47. Jukumu kuu la mahakama ni lipi?

A. kutunga sheria zinaotawala nchi

B. kuhakikisha kuwa haki na usawa umedumishwa

C. kuadhibu wanaovunja sheria

D. kuhakikisha kuwa maendeleo yamefika mashinani kwa wananchi

48. Kila idara ya serikali huongozwa na

A. hakimu

B. kiongozi wa mahakama

C. katibu mkuu

D. spika wa bunge

49. Kazi kuu ya wafanyakazi wa serikali kama vile polisi na wanajeshi ni

A. kuadhibu wanaovunja sheria

B. kuhakikisha kuwa sheria zilizowekwa zimefuatwa

C. kutema wafanyi kazi wa serikali

D. kutunga sheria za kuongoza nchi

50. Kichwa mwafaka kwa kifungu hiki ni

A. Maendeleo katika taifa la Kenya

B. Utekelezaji wa sheria za nchi

C. Bunge la taifa la Kenya

D. Serikali ya Jamhuri ya Kenya

Compiled & supplied by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com